**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI**

OFISI YA RAIS – MAENDELEO YA VIJANA

KATIKA KIKAO NA WADAU WA MAENDELEO YA VIJANA NCHINI

**TAREHE 27 APRILI 2026 DAR ES SALAAM**

Ndugu washiriki, napenda kuwatambua kwa itifaki kama ifuatavyo:

- **Ndugu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana,**
- **Naibu Katibu, Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana,**
- **Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es salaam**
- **Wakurugenzi kutoka Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana**
- **Afisa vijana wa Mkoa,**
- **Viongozi wa mashirika ya kiraia na asasi za vijana/wawakilishi wa Sekta Binafsi; washirika wa maendeleo;**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Mabibi na Mabwana.**
- **wageni wote waalikwa.**

***VIJANA TUYAJENGE …… TANZANIA NI YETU***

***Nawakaribisha sana.***

**Ndugu washiriki,**

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika kikao hiki muhimu kinachowakutanisha wadau wa maendeleo ya vijana nchini. Kikao hiki ni cha kimkakati na cha msingi katika kuimarisha uelewa wa pamoja, kujenga mshikamano wa wadau, na kuweka mwelekeo wa pamoja katika utekelezaji wa ajenda ya maendeleo ya vijana nchini.

Kipekee kabisa, kikao hiki kinafanyika katika kipindi ambacho Serikali imechukua hatua ya kihistoria ya kuanzisha Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana mahsusi kwa ajili ya kushughulikia masuala ya vijana kwa mtazamo wa kitaifa, jumuishi na wa kimkakati zaidi.

**Ndugu washiriki,**

Kuanzishwa kwa Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana ni uamuzi wa kimkakati unaotokana na uelewa mpana kuwa vijana inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 34.5 ya idadi ya watu nchini na ndio nguvu kazi kuu ya Taifa. Uwekezaji kwa vijana ni uwekezaji wa moja kwa moja katika ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na mustakabali wa Taifa.

Kabla ya kuanzishwa kwa Ofisi hii, kulikuwepo na changamoto za mgawanyiko wa majukumu ya masuala ya vijana katika taasisi mbalimbali, ukosefu wa uratibu wa kitaifa, pamoja na ufinyu wa mifumo jumuishi ya utekelezaji. Hali hii imekuwa ikisababisha changamoto mbalimbali katika ufanisi na athari za juhudi mbalimbali zilizokuwa zikifanywa.

Kwa mantiki hiyo, Serikali imeanzisha Ofisi hii kama kitovu cha uratibu, sera, usimamizi na ufuatiliaji wa masuala yote ya maendeleo ya vijana nchini, kwa lengo la kuhakikisha kuwa jitihada zote zinaelekezwa kwa pamoja na kuleta matokeo yenye tija.

**Ndugu washiriki,**

Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana imepewa majukumu ya msingi yanayolenga kuleta mabadiliko ya kimfumo na kiutendaji katika maendeleo ya vijana. Majukumu hayo ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana yam waka 2007 toleo mwaka 2024 pamoja na sera, mikakati na mipango yote inayolenga kukuza ustawi wa vijana, kuandaa na kusimamia mifumo ya kitaifa ya uratibu wa masuala ya vijana, pamoja na kuhakikisha muunganiko madhubuti kati ya sera, mipango na utekelezaji katika ngazi zote za Serikali.

Aidha, Ofisi hii inasimamia uwezeshaji wa kiuchumi kwa vijana kupitia ajira, ujasiriamali na ubunifu; kuimarisha ushiriki wa vijana katika uongozi na michakato ya maamuzi; pamoja na kusimamia ustawi wa vijana ikiwemo afya ya akili, maadili na maendeleo ya kijamii. Vilevile, Ofisi ina jukumu la kuimarisha ushiriki wa vijana katika majukwaa ya kikanda na kimataifa na kuhakikisha uwepo wa mifumo madhubuti ya ufuatiliaji na tathmini ya programu za vijana nchini.

**Ndugu washiriki,**

Katika kipindi kifupi tangu kuanzishwa kwake, Ofisi imeanza kutekeleza majukumu yake kwa kasi na mwelekeo wa kimkakati. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuandaa na kuboresha muundo wa taasisi ili kuimarisha ufanisi wa kiutendaji, kuanza maandalizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Uratibu wa Masuala ya Vijana, pamoja na kuendelea na uchambuzi wa hali halisi wa Vijana, Amani na Usalama.

Sambamba na hilo, Serikali imeanzisha na kuimarisha Majukwaa ya Vijana katika maeneo mbalimbali ya nchi, hatua iliyosaidia kuongeza ushiriki wa vijana katika mijadala ya maendeleo. Aidha, imeanzishwa Youth Call Center inayowawezesha vijana kutoa maoni, changamoto na mapendekezo yao kwa wakati, na hivyo kuimarisha uwazi na uwajibikaji. Pia, maboresho ya miongozo ya stadi za maisha na viwango vya ufundishaji kwa vijana yanaendelea kutekelezwa kwa lengo la kuboresha ubora wa maendeleo ya vijana.

**Ndugu washiriki,**

Kupitia hatua hizi, mafanikio ya awali yameanza kuonekana. Yakiwemo kuongezeka kwa ushiriki wa vijana katika majukwaa ya maendeleo, kuimarika kwa mawasiliano kati ya Serikali na vijana, pamoja na kuongezeka kwa upatikanaji wa taarifa na fursa kwa vijana.

Aidha, ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi na wadau wa maendeleo umeanza kuimarika, jambo linaloonesha kuwa msingi wa utekelezaji jumuishi umeanza kujengwa.

**Ndugu washiriki,**

Pamoja na mafanikio hayo, bado tunakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo ukosefu wa ajira kwa vijana, ufinyu wa mitaji na masoko, pamoja na ujuzi usioendana na mahitaji ya soko la ajira. Aidha, changamoto za afya ya akili na mienendo hatarishi zinaendelea kuhitaji umakini maalum.

Hata hivyo, changamoto hizi pia zinatoa fursa kubwa za uwekezaji katika uchumi wa kidijitali, ubunifu na teknolojia, sekta za uzalishaji, pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kitaifa na kimataifa katika maendeleo ya vijana.

**Ndugu washiriki,**

Serikali inaendelea kutekeleza afua mbalimbali zikiwemo utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kupitia Halmashauri, programu za mafunzo ya ujuzi na ajira, pamoja na kukuza ubunifu, ujasiriamali na mifumo ya incubation kwa vijana. Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya sera, sheria na miongozo ili kuhakikisha utekelezaji wenye tija na endelevu.

Kwa siku zijazo, Serikali imejipanga kupanua fursa za ajira na ujasiriamali, kuimarisha uchumi wa kidijitali, kukuza uwekezaji katika ubunifu na teknolojia, pamoja na kuimarisha mifumo ya data na ushahidi kwa ajili ya maamuzi sahihi ya kisera. Hatua hizi zote zinalenga kuhakikisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 pamoja na mipango ya maendeleo ya Taifa unafikiwa kwa ufanisi.

**Ndugu washiriki,**

Maendeleo ya vijana si jukumu la Serikali pekee bali ni jukumu la wadau wote na ni suala mtambuka ambalo haliwezi kufanikiwa kupitia jitihada za upande mmoja pekee, bali linahitaji uwajibikaji wa pamoja. Wakati Serikali ikiendelea kujenga msingi imara wa kisheria na kisera, mafanikio ya kweli yanategemea nguvu ya sekta binafsi katika kuzalisha fursa za ajira, pamoja na mchango wa mashirika ya kiraia katika kutoa elimu ya stadi za maisha na kutetea haki za vijana kuanzia ngazi za chini. Kuna umuhimu wa kuunganisha rasilimali fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo na maarifa ya kitaaluma kutoka taasisi za elimu ili kuhakikisha kuwa vijana wanaandaliwa kulingana na mahitaji halisi ya soko la ajira na mabadiliko ya teknolojia duniani.

Maendeleo ya vijana yanapaswa kutazamwa kama uwekezaji wa kijamii ambapo kila mdau ana wajibu wa kimaadili na kisheria kuchukua hatua mahususi katika eneo lake. Kupitia ushirikiano huo thabiti, taifa litatengeneza mfumo utakaomwezesha kila kijana kupata fursa stahiki, jambo ambalo hatimaye litachochea ukuaji wa uchumi wa taifa na kuimarisha utangamano wa kijamii kwa kutumia ipasavyo nguvu kazi ya vijana.

Hivyo, nitoe wito kwa Wizara, Idara na Wakala, sekta binafsi, mashirika ya kiraia, washirika wa maendeleo pamoja na taasisi za elimu kuendelea kushirikiana na Serikali katika kutekeleza sera, mikakati, programu na afua za maendeleo ya vijana.

**Ndugu washiriki,**

Kuanzishwa kwa Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana ni mwanzo wa enzi mpya ya usimamizi wa masuala ya vijana nchini. Ni imani yangu kuwa kupitia ushirikiano wetu, tutafanikiwa kujenga kizazi cha vijana wenye uwezo, ubunifu na mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa letu.

Naomba kutumia kikao hiki kama jukwaa la kujadiliana kwa kina, kubadilishana uzoefu na kutoa mapendekezo yatakayosaidia kuboresha zaidi utekelezaji wa ajenda ya maendeleo ya vijana nchini.

***Asanteni sana kwa kunisikiliza.***